SIKU YA UTUMISHI WA UMMA BARANI AFRIKA

1. 0 Utangulizi

Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika ni siku maalum ya Watumishi wa Umma na taasisi za Umma ambayo husherehekewa tarehe 23 Juni kila mwaka na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) kwa lengo la kutambua mchango wa Watumishi wa Umma katika maendeleo ya Bara la Afrika. Chimbuko la Sherehe hizi ni uamuzi wa Mkutano wa Mawaziri wenye dhamana ya Utumishi wa Umma uliofanyika Tangiers nchini Morocco mwaka 1994. Uamuzi huu ulizitaka nchi za Afrika kusherehekea sherehe hizo kwa kauli mbiu moja katika Bara zima la Afrika.

Mkutano wa nne wa Mawaziri wenye dhamana na Utumishi wa Umma uliofanyika tarehe 4 na 7 Mei 2003 2003 nchini Afrika Kusini uliamua kuwa Siku ya Utumishi wa Umma iwe ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Utawala Bora na Utumishi wa Umma chini ya Umoja wa Afrika (AU). Pia, Mkutano wa kamati ya Mawaziri wa Utumishi uliofanyika Windhoek Namibia uliofanyika tarehe 24 Oktoba 2007 ulipitisha uamuzi kuwa kila baada ya miaka miwili nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) kuadhimisha kwa pamoja katika moja ya nchi wanachama itakayokuwa imejitolea kuwa mwenyeji wa sherehe hizo. Kikao cha 15 cha Baraza la Mawaziri la Umoja wa Afrika (AU) kilichofanyika Sirte nchini Libya Tarehe 1

Julai 2009 kiliridhia kanuni hii ya kuadhimisha Siku ya Utumishi wa Umma katika nchi mojawapo mwanachama wa umoja huo kila baada ya miaka miwili.

2.0 Malengo ya Sherehe ya Siku ya Utumishi wa Umma

Malengo ya msingi ya Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika ni kama ifuatavyo:

- Kuwezesha watumishi wa Umma kutambua Dira, Dhima, na Malengo; Programu na Mikakati; na Mafanikio na Changamoto zinazokabili Utumishi wa Umma;
- Kutambua mchango na umuhimu wa Watumishi wa Umma na umuhimu wao katika kuleta maendeleo katika Nyanja mbalimbali katika Taifa;
- Kuhamasisha na kuwapa motisha Watumishi wa Umma waendelee na kazi yao nzuri ya ujenzi wa Taifa na kuendelea kuwa wabunifu ili kutatua changamoto mbalimbali katika jamii;
- Kupata mrejesho kutoka kwa wateja na wadau wao juu ya huduma wanazozitoa; na
- Kuandaa Utumishi wa Umma ili uweze kukabiliana na changamoto mbalimbali ili uweze kuleta maendeleo siku za usoni.

3.0 Historia ya Sherehe ya Siku ya Utumishi wa Umma 3.1 Sherehe za Utumishi wa Umma Tanzania

3.1.1 Mwaka 2003

Hapa nchini, maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yalianza mwaka 2003 kwa kufanyika Kongamano la kujadili hali ya utoaji huduma katika Ofisi

za Serikali na masuala mbalimbali yanayohusu mabadiliko na ufanisi wa huduma katika ofisi hizo.

3.1.2 Mwaka 2005

Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yalianza kufanyika kwa kuwa na maonesho ya taasisi 12 za umma yaliyofanyika katika viwanja vya Karimjee jijini Dar es salaam.

3.1.3 Mwaka 2006

Mwaka 2006 maonesho ya Wiki ya Utumishi yalifanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja. Uamuzi huo ulilenga kuwezesha wananchi wengi zaidi kuhudhuria na kujua taasisi za serikali zinafanya nini ikiwa ni pamoja na kutoa kero zao na kuwasilisha maoni yao kuhusu huduma mbalimbali za serikali.

3.1.4 Mwaka 2007

Mwaka 2007 maonesho yalifanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Jakaya Mrisho Kikwete alikuwa mgeni rasmi. Taasisi za serikali 78 zilishiriki katika maonesho hayo. Mgeni rasmi alitoa ari kwa maonesho hayo kufanyika mikoani ili kutoa nafasi kwa wakazi waliopo mikoani kufahamu kazi zinazotekelezwa na serikali yao.

3.1.5 Mwaka 2008

Sherehe za Wiki ya Utumishi kwa mara nyingine zilifanyika katika viwanja vya Mnazi mmoja. Taasisi za serikali 110 zilishiriki katika maonesho hayo na

kwa mara ya kwanza taasisi hizi zilishindanishwa ili kupata taasisi iliyoonyesha ubunifu katika utoaji huduma.

3.1.6 Mwaka 2009

Mwaka 2009 Tanzania ilikuwa mwenyeji wa sherehe za Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika. Hivyo sherehe za Siku ya Utumishi wa Umma hapa nchini zilifanyika sanjari na Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika, Juni 15, 2009 hadi Juni 23, 2009. Matukio katika sherehe hizo ilikuwa ni Kongamano la siku mbili linalohusu Utumishi wa Umma Barani Afrika lililofanyika Tarehe Juni 17-18, 2010 jijini Dar es salaam katika Hoteli ya Kilimanjaro Kempinski na kuhudhuriwa na baadhi ya Mawaziri wenye dhamana ya Utumishi wa Umma Barani Afrika, Maonesho ya Siku ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika tarehe 15 Juni mpaka 23 Juni katika viwanja vya Mnazi mmoja, na Tuzo za Ubunifu za Maonesho zilizotolewa katika viwanja hivyo tarehe 23 Juni 2009.

3.1.7 Mwaka 2010

Sherehe za Wiki ya Utumishi wa Umma zilifanyika mkoani Mwanza katika viwanja vya Kirumba kuanzia tarehe 16-23 juni 2010. Matukio katika sherehe hiyo yalikuwa ni maonesho yaliyofanyika katika viwanja vya Kirumba na kushirikisha Taasisi za serikali 171 na Tuzo za Ubunifu za Maonesho hayo ambazo zilitolewa kwa Taasisi zilizoonesha ubunifu katika utoaji huduma.

3.1.8 Mwaka 2011

Mwaka 2011 Tanzania ilikuwa mwenyeji wa sherehe za Siku ya Utumishi wa Umma wa Umoja wa Mataifa, Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika. Hivyo sherehe za Siku ya Utumishi wa Umma hapa nchini zilifanyika sanjari na sherehe hizo kuanzia Tarehe Juni 15, 2011 hadi Juni 23, 2011. Matukio katika sherehe hizo ilikuwa ni Kongamano la siku tatu lililohusu Utumishi wa Umma la Umoja wa Mataifa na Bara la Bara la Afrika lililofanyika kuanzia Tarehe Juni 21-23, 2011 jijini Dar es salaam katika Kumbi za Mlimani City, Maonesho ya Siku ya Utumishi wa Umma ya Umoja wa Mataifa, Bara la Afrika na Tanzania yaliyofanyika katika Viwanja vya Mnazi mmoja kuanzia Tarehe 15 Juni mpaka 23 Juni 2011 na Tuzo za Ubunifu za Umoja wa Mataifa zilizofanyika Mlimani City Tarehe 23 Juni 2011, Tuzo za Ubunifu za Bara la Afrika zilizoshirikisha Nchi wanachama sita katika Viwanja vya Mnazi mmoja na Tuzo za Ubunifu kwa Taasisi za hapa nchini zilifanyika katika Viwanja vya Mnazi mmoja na kushirikisha Taasisi 183. Aidha nchi zifuatazo kutoka Bara la Afrika zilishiriki maonesho hayo; Tanzania, Kenya, Zimbabwe, Afrika Kusini, Zambia, na Congo Brazavile.

3.2 Sherehe za Utumishi wa Umma Barani Afrika

Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zimekwisha sherehekea Sherehe za Utumishi wa Umma za Barani Afrika mara tatu kwa kuzingatia maamuzi ya Kikao cha Kamati ya Mawaziri wa Utumishi wa Umma (2007) na Kikao cha Baraza la Mawaziri la Umoja wa Afrika (2009) kama ifuatavyo:

3.2.1 Mwaka 2007 Windhoek Namibia

Sherehe hizi zilifanyika kwa mara ya kwanza Mwezi Oktoba 2007 na zilihudhuriwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika. Kauli mbiu ilikua ni " *Promoting Good Governance with Emphasis on Anti Corruption and Ethics*".

3.2.2 Mwaka 2009 Dar es salaam Tanzania

Sherehe hizi ziliadhimishwa kwa mara ya pili Mwezi Juni 2009 na zilihudhuriwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU). Kauli mbiu zilizotumika kwa maadhimisho hayo zilikuwa ni:

Kauli mbiu kubwa (main theme) ilikua ni:

"Capacity Development for Future Capability of the Public Service" Kauli mbiu ndogo (sub theme) ni:

"*Fostering Partnership and Collaboration for Sustainable Development and Improved Service Delivery in Africa*"

3.2.3 Mwaka 2011 Dar es salaam Tanzania

Sherehe hizi ziliadhimishwa kwa mara ya tatu Mwezi Juni 2011 na kuhudhuriwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika. Kauli mbiu zilizotumika kwa maadhimisho hayo zilikua ni:

Kauli mbiu kubwa (main theme) ilikuwa ni:

"*Transformative Leadership in Public Administration and Innovation in Governance: Creating a better future for all*" Kauli

mbiu ndogo (sub theme) ilikuwa ni:

a) *"The Charter for Values and Principles of Public Service and*

Administration in Africa: A Unique Tool to Enhance Service Delivery"

b) *"Continuous Innovations in Public Services: ICT as an Enabler to Foster e-Government".*

3.2.4 Mwaka 2013 Accra Ghana

Sherehe za Siku ya Utumishi wa Umma kwa mara ya nne zilifanyika katika mji wa Accra nchini Ghana. Kauli mbiu ya Maadhimisho hayo ilikua ni :

Kauli mbiu Kubwa (main theme) ni:

"African Public Service in the Age of Open Government: Giving voice to Citizens"

Kauli mbiu ndogo (sub themes) ni:

a) *Strengthening Citizens Participation and Responsibilities*
b) *Enhancing Accountability, Transparency and Integrity*
c) *Empowering Management Development Institutions to Build Capacity for Service Improvement.*

3.2.5 Matukio katika Sherehe yalikua yafuatayo:

3.2.5.1 Kongamano kuhusu Utumishi wa Umma Barani Afrika

Kongamano lilijadili masuala mbalimbali yanayohusu Utumishi wa Umma Barani Afrika kuendana na Kauli mbiu kubwa na ndogo. Wawezeshaji wa Kongamano hilo walitoka katika nchi mbalimbali Barani Afrika.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma Mh. Celina O. Kombani alikuwa mwenyekiti wa mpito wa Mawaziri wenye dhamana na Utumishi wa Umma Barani Afrika wakati wa maadhimisho hayo jijini Accra.

3.2.5.2 Maonesho

Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) zilifanya maonesho ya huduma mbalimbali za umma zinazotolewa na taasisi ndani ya nchi zao kwa kuzingatia kauli mbiu kubwa na ndogo.

3.2.5.3 Maandamano

Maandamano yalifanyika kutoka katika mji ya wa Accra hadi eneo la maonesho ambalo lilikua viwanja vya Bunge. Washiriki walipimwa afya baada ya matembezi.

3.2.5.4 Kutembelea vivutio vya Utalii

Siku moja maalum ilitengwa ili kuwezesha waalikwa kutoka nchi zinazoshiriki kutembelea vivutio vya Utalii nchini Ghana.

3.2.5.5 Tuzo na Sherehe maalum ya kuagwa waalikwa

Sherehe maalum ya kutoa tuzo na kuwaaga wageni kutoka nchi za Afrika ilifanyika Terehe 23 Juni jioni katika ukumbi wa Bunge la Ghana.

Banda la Tanzania lilipata tuzo katika maeneo yafuatayo;

- Tuzo ya Ubunifu katika Utoaji Huduma (Best Innovation in Service Delivery), Tuzo ilichukuliwa na Wakala ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)
- Tuzo ya Taasisi inayosimamia Kazi zake Vizuri (Best Managed Organisation), Tuzo hii ilichukuliwa na Ofisi ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (NAO), na
- Tuzo ya Taasisi Bora katika Uwajibikaji na Uwazi (Most Accountable & Transparent Organisation), Tuzo hii ilichukuliwa na Wakala ya Vipimo (WMA).

4.0 Mwaka 2014

Maadhimisho yalifanyika katika viwanja vya Mnazi mmoja jijini Dar es salaam. Kaulimbiu kwa mwaka 2014 ilikua ni "**Mkataba wa Misingi na Kanuni za Utumishi wa Umma Barani Afrika ni Chachu ya Kuimarisha Utawala Bora na Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi**"

Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Ombeni Y. Sefue alikabidhi zawadi kwa Taasisi zifuatazo zilizofanya vyema zaidi;

4.1 BANDA BORA

(I) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

(II) Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA).

(III) Wizara ya Maji.

4.2 MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI MAHALI PA KAZI (I)

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

(II) Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.

(III) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania.

4.3 UBUNIFU KATIKA KUBORESHA UTOAJI HUDUMA

(I) **Wizara ya Maji** – washindi kupitia Teknolojia ya kupunguza madini ya floride katika maji kwa kutumia mifupa ya ng'ombe.

(II) **Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)**-washindi wa pili kupitia kifaa kiitwacho Umeme tayari "*ready Board*" kinachowezesha wananchi kupata umeme bila kusuka na kusambaza nyaya umeme (wiring) katika nyumba.

(III) **Wakala ya Vipimo (WMA)**-washindi wa tatu kupitia mfumo wa kieletroniki *"Clock in and clock out task information system"* unaotumika kudhibiti muda wa kuingia na kutoka kazini.

5.0 Mwaka 2015

Maadhimisho yanafanyika katika viwanja vya Mnazi mmoja jijini Dar es Salaam. Kauli mbiu ya maadhimisho ni **"Utumishi wa Umma katika Bara la Afrika ni Chachu ya Kuwawezesha Wanawake, Kuongeza Ubunifu na Kuboresha Utoaji Huduma kwa Umma"**

Aidha, kaulimbiu hii itatumika katika maadhimisho ya Kibara katika nchi ya Kongo Brazaville.

6.0 Ushiriki wa Tanzania Kibara

Mwaka 2013 Tanzania ilikua Mwenyekiti wa Mpito wa Mkutano wa Mawaziri wenye Dhamana na Utumishi wa Umma Barani Afrika (CAMPS) na Kinara wa Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika.

Imeandaliwa na:

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,

Kny: Katibu MKuu, Ofisi ya Rais (UTUMISHI) Mei 2015.